



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE



Tarehe: 17/01/2022

TANGAZO LA AJIRA YA MKATABA YA KAZI ZA UFUNDI KWA AJILI YA UJENZI  
WA JENGO LA WAGONJWA WA DHARURA (EMERGENCY MEDICAL  
DEPARTMENT) NA NYUMBA YA WATUMISHI (THREE IN ONE) KATIKA KITUO  
CHA AFYA KYIMO

ZABUNI NA. LGA/071/2021/2022/RDC/W/28 LOT I & II

1. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe anawatangazia wananchi wote kwamba Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe imepokea fedha kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa jengo la Wagonjwa wa dharula (EMD) katika Hospitali ya Wilaya Tukuyu na Ujenzi wa Nyumba za Watumishi (Three in One).
2. Hivyo basi, Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya inakaribisha kazi za Mikataba ya Muda Mfupi za Mafundi wenye sifa na uzoefu katika shughuli za Ujenzi ambao utafanyika kwa njia ya Manunuzi ya "Force Account" kwa majengo yafuatayo:-

Lot Na.	Jina la Mradi	Kazi kuu zitakazofanyika
I	Ujenzi wa jengo la Wagonjwa wa dharula (EMD) katika Hospitali ya Wilaya Tukuyu	Ufundi Uashi, Uchomeleaji wa vyuma, kusuka nondo, usuukaji na ufungaji wa mifumo ya umeme na TEHAMA (ICT), Mifumo ya maji safi na taka, upigaji rangi, uwekaji marumaru na terrazzo kwa baadhi ya sehemu za ndani ya jengo n.k
II	Ujenzi wa Nyumba za Watumishi (Three in One)	Ufundi Uashi, usuukaji na ufungaji wa mifumo ya umeme una Mifumo ya maji safi na taka, upigaji rangi, uwekaji marumaru n.k

3. Hivyo basi, wanahitajika mafundi ujenzi wenye sifa katika fani zifuatazo:-

i. **Fundi Uashi**

- Awe na elimu ya ufundi Uashi/ujenzi na mwenye kujua kusoma ramani za majengo

